

## Enrolment policy - Swahili

# Sera ya Kujiandikisha

Maelezo kwa wazazi

Sera ya Kujiandikisha kwa Wanafunzi katika Shule za Serikali ya NSW ipo ili kusaidia shule kutosheleza jukumu zao chini ya *Sheria ya Elimu 1990* – ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi ana mahali hapo shule yake ya mtaa. Sera pia inawaonyesha wafanyakazi ikiwa pamoja na jamii njia wazi ya kuandikisha.

## Kwa nini sera ya kujiandikisha imepitiwa?

Jimbo mzima, jamii nyingi zinabadilika. Zingine zinazidi kwa kiasi ambacho hakujawahi kamwe kuonekana. Shule nyingine ambazo zilizoea kuweza kukubali kujiandikisha kwa nje-ya-eneo, hazina nafasi ili kufanya hivyo bado.

Sera iliyopitishwa imebuniwa ili kusaidia shule kusimamisha maombi yote ya kusajili, kutia moyo uthabiti zaidi katika kufanya uamuzi pamoja na kuhakikisha kuwa uchaguzi wa kusajili unaeleweka na wazazi.

## Mabadiliko ni nini?

### The enrolment cap

The enrolment cap (mwisho wa kusajili) ni idadi ya wanafunzi ambao wanaweza kujiandikisha shule fulani kulingana na maafikiano ya kudumu ya shule. The enrolment cap inatuambia kama shule inaweza au haiwezi kuwa na nafasi za kutosha ili kukubali kusajili kwa nje-la-eneo. Hiyo sio lengo au kikomo kwa idadi ya kusajili kwa mtaa ambako shule inaweza kuchukua.

Kila shule ambayo ina eneo la mtaa la kiingizo itakuwa na cap inayoamuliwa na idara kuanzia Term (Muhula) 4 2019.

Katika the enrolment cap, idadi fulani ya nafasi ya kusajili lazima itunzwe kwa idadi ya kufaa ya wanafunzi wa mtaa ambao watahitaji kusajili mnamo mwaka. Mahali pa kusajili panapotunzwa panaitwa the buffer (bafa). Kwa sababu hiyo, shule haitachukua wanafunzi ambao wametoka nje ya mtaa ikifika the buffer, ila kuwe na hali maalum.

### Ukaguzi wa anwani ya makazi wa pointi-100

Wazazi wanaopanga kusajili mtoto wao kwa shule ambayo ipo karibu ya buffer au cap yake au imeshafika buffer au cap yake wataombwa kujaza ukaguzi wa anwani ya makazi wa pointi-100 ili kuhakikisha kuwa wanaishi ndani ya eneo la kiingizo la mtaa lilionyeshwa la shule. Hii inamaanisha kuwa wazazi watahitaji kutoa hati ili kuhakikisha anwani ya mtoto ya sasa hivi.

Ili shule ziweze kutafuta maelezo pekee yanayohusu kusajili kwa mtoto, orodha ya hati zilizokubaliwa kwa ukaguzi wa anwani ya makazi inapatikana shuleni au kwenye tovuti ya idara kwenye https://education.nsw.gov.au/policy-library/policies/enrolment-of-students-in-nsw-government-schools.

### Vigezo vya kuchaguliwa kwa kusajili kwa nje-eneo

Kusajili kwa ndugu wa mama mmoja ni kipaumbele kabisa sikuhizi (panapowezekana) pamoja na vigezo vya kuchaguliwa kwa kusajili nje-la-eneo havitakuwepo ikiwemo ni pamoja na uwezo, tendo kuu au mafanikio ya mwanafunzi.



NSW GOVERNMENT

## Nini hakijabadilika?

Shule zitaendelea kusajili wanafunzi ambao wanakaa katika eneo la kiingizo la mtaa, bila kujali, hali ya cap ya shule.

Hakuna mabadiliko kwa haki za kujiandikisha kwa wanafunzi wa nje-ya-mtaa. Katika shule ambazo zilizo na nafasi za kupatikana, kila ombi la kusajili litafikiriwa kulingana na ustahili wake. Ikiwa shule ipo chini ya kujazwa kabisa, maombi ya nje-la-eneo kwa ndugu wa mama mmoja wa wanafunzi wa sikuhizi yatapata kipambele cha kusajili.

Shule zitaendelea kutoa msaada na ushauri kwa familia wakati wa mfuatano wa kusajili, ikiwa pamoja na makadirio ya hali maalum na ya kuvuta sana haswa kwa wanafunzi na familia ambao wana hali ngumu ya kimaisha.

Shule zitaendelea pia kutekeleza sera kwa usawa na uthabiti kwa kutumia maendeleo wazi pamoja na yenye kuhusika wakati wanapoamua maamuzi kuhusu maombi ya kujisajili. Wazazi wana haki ya rufaa ili kuamua kama mfuatano uliotajwa umetumiwa kwa njia sawa kufuatana na taratibu.

## Lakini mabadiliko yana maana gani kwangu?

### Vipi ikiwa mtoto wangu ameshajiandikisha tayari lakini sisi hatuishi katika eneo la kiingizo la shule?

Mtoto wako ataendelea kuandikishwa shuleni kwa sababu sera iliyopitiwa haihusu wanafunzi ambao wameshasajili katika shule za Serikali ya NSW.

### Tulikuwepo hapa eneo wakati mtoto wangu aliposajiliwa shuleni. Idara imebadilisha mpaka wa shule tangu muda ule na sasa makazi yetu yapo nje ya eneo. Nina watoto wengine na nataka wote waende shule sawa. Uchaguzi wangu ni nini?

Wakati wengine ni lazima idara kufanya urekebishaji kwenye eneo la kiingizo cha kusajili la mtaa wa shule. Hii inaweza kumaanisha kuwa familia yenye mtoto au watoto ambao wameshasajiliwa ndiyo wapo nje ya eneo la kiingizo la mtaa. Wakati hiyo ikitokea, familia wataweza bado kusajili ndugu wa mama mmoja pamoja shuleni, bila kujali kama shule imepita buffer au cap.

### Nina mtoto ambaye ameshasajiliwa tayari kama mwanafunzi wa nje-eneo katika shule ya Serikali ya NSW. Je, niweze kusajili watoto wangu wengine pale shule ileile pia?

Kufanya hivi kutategemea uwezo wa shule:

- Ikiwa shule **siyo karibu ya buffer yake**, ndipo ndugu wa mama mmoja waweze kusajili pale shuleni. Kwa kweli, ndugu wa mama mmoja wa wanafunzi ambao wameshasajili tayari watapewa kipaumbele, inapowezekana, kupita maombi mengine ya kusajili kwa nje-ya-mtaa.
- Ikiwa shule ni **karibu buffer yake**, ndipo shule itaanzisha paneli ya kusajili nje-eneo. Paneli hufikiria maombi ya kusajili kwa nje-eneo wakati idadi ya maombi ya nje-eneo yanayopokewa inazidi idadi ya nafasi inayopatikana chini ya buffer. Tena, kwa mfano huu, ndugu wa mama mmoja wa wanafunzi ambao wamesajiliwa kwa sasa hivi watakuwa kipaumbele, inapowezekana, kupitia maombi mengine ya kusajili kwa nje-ya-eneo.
- Ikiwa shule **imejazwa kabisa, yani tele**, haitakubali maombi ya kujisajili kwa nje-ya-eneo ila ikiwa kuna hali maalum.

### Mimi nimeshakubali ahadi ya mtoto wangu kwenda shule mwakani 2020 ambayo siyo shule yangu ya mtaani. Nini itatokea sasa?

Kusajili kule kutaendelea. Kusajili kwa nje-ya-eneo ambako kulikubaliwa kabla Term 4 2019 kwa wanafunzi wanaoanza katika 2020 hakutaathirika.

### Nini ni vigezo kwa kujisajili katika shule ambayo siyo shule yangu ya mtaa?

Shule ambazo zinaweza kukubali maombi ya kusajili ya nje-ya-eneo zinaanzisha paneli ya uchaguzi wa kusajili kwa nje-ya-eneo, kama mahitaji yapo zaidi idadi ya nafasi chini buffer ya shule.

Shule zinahitajika kufanyiza vigezo vya uchaguzi kupatikana kwa jamii ya shule.

### Hali zangu ni changamoyo na naona shule hii ni nzuri zaidi kwa mtoto wangu. Tunakaa nje ya eneo la kiingizo cha shule. Nifanye nini?

Sisi tunaelewa kuwa hali za kila mtu siyo sawa, na kuna mifano ambayo hali maalum ikiwemo pamoja na hali za kulazimisha zitahitajika kufikiriwa.

Ikiwa hivi vinahusu, uongee na mwalimu mkuu wa shule ya mtaa wako.

## Mawasiliano

Kwa maswali ya jumla wasiliana kwa: 1300 679 332 au tumia baruapepe: DoEinfo@det.nsw.edu.au

Kwa maswali ya kusajili, ongea na shule la mtaa wako. Pata habari za mawasiliano ya shule kwenye: https://education.nsw.gov.au/public-schools/going-to-a-public-school/finding-a-public-school

## Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji mkalimani ili kukusaidia wasiliana na shule, tafadhali pigia simu Huduma ya Ukalimani wa Simu kwa nambari 13 14 50 na uombe mkalimani katika lugha yako. Umwambie mpokezi simu nambari ya simu unayotaka kupigia simu na mpokezi simu atapata mkalimani kwenye laini ili kukusaidia wewe na mazungumzo. Hutalipa kwa huduma hii.